

Nitapokeaje NDIS

katika WA?

Hatua ya 1



Angalia matakwa ya Ustahili

Angalia matakwa ya Ustahili

Hakikisha ustahili wako katika mtandao: http://www.dsc.wa.gov.au/Am_I_Eligible/

AU piga simu 1800 996 214; TTY (Kichapishaji cha Tele - teletypewriter) 08 9426 9315

AU wasiliana na ofisi ya Uratibu wa Mitaa iliyo karibu nawe (unaweza kupiga simu 08 9489 8900 kwa maelezo zaidi)

Hatua ya 2



Kutoa Nyaraka

Utaunganishwa na Mratibu wa Mitaa ambae atakusaidia na mambo yote yanayohusu kupokea msaada kutoka kwa NDIS. Atahakikisha kama unastahili kabla ya kuanzisha mpango wowote.

Huenda ukahitaji kutoa nyaraka zinginezo kwa mfano taarifa ya matibabu, nakala ya pasipoti au cheti cha kuzaliwa na ushahidi wa anwani unapoishi kupitia kwa Leseni ya Dereva au bili. Unaweza kumuomba mtu akusaidia, kwa mfano rafiki, mtu wa familia au wakili.

Hatua ya 3



Mipango ya Misaada

Ukisubiria uhakikisho wa ustahili, labda ungependa kuwasiliana na mashirika ambao yanafadhiliwa wakueleze Zaidi kuhusu mchakato wa mipango au uwaulize wale ambao wanakuhudumia kwa sasa wakusaidie.

Mashirika yanayofadhiliwa ni pamoja na: Developmental Disability WA, Down Syndrome WA, Far North Community Service, Fremantle Multicultural Centre, Richmond Wellbeing, WAIS na WA Deaf Society (ikiungwa mkono na Idara ya Jamii – Huduma za Ulemavu [Department of Communities – Disability Services]). Kama umetambuliwa kuwa na Ugonjwa wa Twahahudi, unaweza kuwasiliana na Chama cha Tawahudi [Autism Association].

Hatua ya 4



Mipango ya Msaada binafsi inaanza

Baada ya ustahili wako kuhakikishwa, Mratibu wa Mitaa atakusaidia kuanzisha mpango binafsi unaokufaa. Unaweza kumuomba mtu akusaidie kwa haya, kwa mfano rafiki, mtu wa familia, mtunzaji au wakili. Mara tu ikipitishwa, Mipango ya Kufaa Kila mtu binafsi huanza kwa kipindi cha miezi kumi na miwili, 12.

Tukiungwa Mkono na Idara ya Jamii (Huduma za Ulemavu)